JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

Simu: +255262963470
Nukushi: +255262963117
Barua pepe: ps@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz

Mji wa Serikali,

Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S. L. P 2996,
**40478 DODOMA**.

## TAARIFA KWA UMMA

## MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA MUHIMU NCHINI

### A. UTANGULIZI

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inashirikiana na Tume ya Ushindani (FCC) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kutekeleza jukumu la kufuatilia na kufanya tathmini ya mwenendo wa bei za bidhaa muhimu nchini. Taarifa ya leo ni mwendelezo wa utaratibu wa kutoa taarifa za kila mwezi kufuatia tathmini iliyofanywa na Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Ninapenda kupongeza juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi imara wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, za kuendelea kuweka mazingira rafiki ya biashara nchini. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuondoa baadhi ya kodi na kutoa ruzuku kwenye mafuta ya petroli na dizeli ili kuleta unafuu wa bei kwenye soko. Hata hivyo, kuanzia mwanzoni mwa mwezi Septemba hali ya upatikanaji wa mafuta ya petroli na dizeli kwenye soko la dunia imeendelea kuimarika ambapo bei za bidhaa hizo zimeshuka na hivyo kupunguza gharama za usafirishaji na usambazaji wa bidhaa. Kutokana na hali hiyo, tunatarajia katika siku zijazo bei za bidhaa nchini zitaendelea kushuka na kuleta unafuu katika soko la ndani.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Matokeo ya tathmini iliyofanywa katika kipindi cha mwezi Agosti 15 hadi Septemba 15, 2022 imebainisha ongezeko dogo katika baadhi ya bidhaa za vyakula hususan mchele, mahindi, na maharage. Kupanda kwa bei za bidhaa hizo ni kutokana na uhaba wa mvua kwenye maeneo mengi katika msimu wa kilimo wa mwaka 2021/2022 uliosababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao hayo.

**Ndugu Waandishi wa Habari:**

Takwimu za bei za baadhi ya mazao ya chakula zinakusanywa kutoka kwenye masoko mbalimbali kwenye Mikoa yote ya Tanzania Bara kupitia Wakusanya Taarifa za Masoko (Market Monitors). Aidha, taarifa za bei za baadhi ya bidhaa muhimu kama vile bidhaa za vyakula, vifaa vya ujenzi na bidhaa nyingine zinakusanywa kwa kutumia Maafisa Biashara wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini. Vilevile, kila mwezi Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inakusanya taarifa za bei kutoka kwenye masoko yaliyopo katika Mikoa yote ya Tanzania Bara kwa lengo la kukokotoa kiwango cha mfumuko wa bei kwa mwezi husika. Bei za bidhaa kwa kila Mkoa hupatikana kwa kukokotoa wastani wa bei za mazao na bidhaa hizo kutoka kwenye masoko yaliyopo kwenye Mikoa hiyo.

## B. MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA MBALIMBALI

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

### I. VIFAA VYA UJENZI

Uzalishaji wa saruji kwa mwaka 2020/21 ulikuwa tani 6,496,000. Aidha, kwa mwaka 2021/2022 uzalishaji wa saruji umeongezeka kwa asilimia 0.5 hadi tani 6,531,000. Vilevile, uzalishaji wa nondo kwa mwaka 2020/21 ulikuwa tani 278,000; na kwa mwaka 2021/2022 uzalishaji wa nondo uliongezeka kwa asilimia 4.7 hadi tani 291,000. Pia, uzalishaji wa bati kwa mwaka 2020/21 ulikuwa tani 108,000; na kwa mwaka 2021/2022 uzalishaji wa bati uliongezeka kwa asilimia 5.6 hadi tani 114,000. Kiuchumi tunasema soko letu la vifaa vya ujenzi linakua na hii ni dalili njema kwenye uchumi wa mtu mmoja mmoja na Uchumi jumla wa Taifa letu.

**Bei za Bidhaa muhimu za Ujenzi**

**(a) SARUJI:** Bei ya saruji kwa mfuko wa Kilo 50 ni kati ya Shilingi 14,600 na 23,000. Bei hiyo haina mabadiliko ikilinganishwa na bei ya saruji kwa mwezi Agosti. Aidha, bei za chini za saruji zipo kwenye mikoa ya Mtwara, Tanga, Lindi, Dar es Salaam na Kilimanjaro ambayo ni mikoa iliyo karibu na viwanda vya saruji. Bei za juu za saruji zipo kwenye mikoa ya Kigoma, Kagera, Mara,

Simiyu na Mwanza kutokana na umbali wa mikoa hiyo kutoka kwenye viwanda na gharama za usafirishaji.

**(b) NONDO:** Bei ya nondo mm12 ni kati ya Shilingi 23,000 na 28,000 kwa mwezi Septemba. Bei hiyo imeshuka kutoka kati ya Shilingi 24,500 na 30,000 kwa mwezi Agosti. Bei za chini zipo kwenye mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Bei za juu za nondo zipo kwenye mikoa ya Njombe, Songwe, Rukwa na Katavi kutokana na umbali kutoka viwandani na gharama za usafirishaji.

**(c) BATI:** Bei ya bati nyeupe za geji 30 ni kati ya Shilingi 21,000 na 32,500 kwa mwezi Septemba. Ikilinganishwa na bei ya kati ya Shilingi 22,000 na 28,500 kwa mwezi Agosti. Bei ya chini ya bati nyeupe ya mwezi Septemba ipo kwenye Mkoa wa Pwani na bei ya juu ipo kwenye Mikoa ya Njombe na Kigoma.

## II. BIDHAA ZA VYAKULA

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

### (a) MAHINDI

Uzalishaji wa mahindi kwa mwaka 2020/21 ulikuwa tani 7,039,064 na mahitaji yalikuwa tani 5,978,257 hivyo nchi ilikuwa na ziada ya mahindi ya tani 1,060,807. Aidha, kwa mwaka 2021/2022 uzalishaji wa mahindi ulishuka kwa asilimia 7.1 hadi tani 6,537,203 na mahitaji yaliongezeka kwa asilimia 0.9 hadi 6,034,943. Hivyo, ziada ya mahindi ilipungua kwa asilimia 56.6 hadi tani 502,260.

Bei ya mahindi kwa mwezi Septemba ni kati ya Shilingi 900 na 1,550 kwa kilo ikilinganishwa na Shilingi 700 hadi 1,500 kwa mwezi Agosti. Aidha, bei ya chini ya mahindi ipo katika mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Manyara na Ruvuma. Bei ya juu ya mahindi ipo katika mikoa ya Pwani na Kagera.

### (b) UNGA WA MAHINDI

Bei ya unga wa mahindi ni kati ya Shilingi 1,250 na 2,000 kwa kilo kwa mwezi Septemba ikilinganishwa na Shilingi 1,400 hadi 1,700 kwa mwezi Agosti. Bei ya chini ya unga wa mahindi ipo katika mikoa ya Iringa, Rukwa na Ruvuma. Bei ya juu ya unga wa mahindi ipo katika mikoa ya Kagera, Mara, Pwani, Shinyanga na Arusha.

**(c) MCHELE**

Uzalishaji wa mchele kwa mwaka 2020/21 ulikuwa tani 2,686,829 na mahitaji yalikuwa tani 1,095,743 hivyo nchi ilikuwa na ziada ya mchele ya tani 1,591,089. Aidha, kwa mwaka 2021/2022 uzalishaji wa mchele ulishuka kwa asilimia 30.9 hadi tani 1,856,731 na mahitaji yalikuwa tani 1,065,534. Hivyo, ziada ya mchele ilishuka kwa asilimia 50.3 hadi tani 791,198.

Bei ya mchele ni kati ya Shilingi 2,000 hadi 3,500 kwa kilo kwa mwezi Septemba; Ikiwa imepanda kutoka kati ya Shilingi 1,700 na 3,000 kwa mwezi Agosti. Bei ya chini ya mchele kwa mwezi Septemba ipo katika mikoa ya Shinyanga, Simiyu na Kigoma. Bei ya juu ya mchele ipo katika mikoa ya Kagera, Dodoma, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Manyara, Singida na Arusha.

**(d) MAHARAGE**

Uzalishaji wa maharage kwa mwaka 2020/21 ulikuwa tani 1,428,434 na mahitaji yalikuwa tani 553,791 hivyo nchi ilikuwa na ziada ya maharage ya tani 879,643. Aidha, kwa mwaka 2021/2022 uzalishaji wa maharage ulishuka kwa asilimia 11.1 hadi tani 1,269,487 na mahitaji yalikuwa tani 488,753. Hivyo, ziada ya maharage ilishuka hadi tani 780,734.

Bei ya maharage ni kati ya Shilingi 1,750 na 3,500 kwa kilo kwa mwezi Septemba; ikiwa imepanda kutoka kati ya Shilingi 1,800 na 2,600 kwa kilo mwezi Agosti. Bei ya chini ya maharage kwa mwezi Septemba ipo katika mikoa ya Katavi, Morogoro, Songwe, Kilimanjaro na Mbeya. Bei ya juu ya maharage ipo katika mikoa ya Dar es Salaam na Arusha.

**(e) VIAZI MVIRINGO**

Bei ya viazi mviringo ni kati ya Shilingi 500 na 1,500 kwa kilo kwa mwezi Septemba. Bei ya viazi haijaonesha mabadiliko ikilinganishwa na mwezi Agosti. Bei ya chini ya viazi mviringo kwa mwezi Septemba ipo katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Manyara. Bei ya juu ya viazi mviringo ipo katika mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Arusha na Mara.

**(f) ULEZI**

Bei ya ulezi ni kati ya Shilingi 1,600 na 3,000 kwa kilo kwa mwezi Septemba. Bei ya chini ya ulezi imepanda kwa Shilingi 400 ikilinganishwa na mwezi Agosti. Bei ya chini ya ulezi kwa mwezi Septemba ipo katika mikoa ya Morogoro na Ruvuma; na bei ya juu imeripotiwa kwenye mikoa ya Kagera na Shinyanga.

**(g) MAFUTA YA KUPIKIA**

Bei ya mafuta ya kupikia ya alizeti ni kati ya Shilingi 5,000 na 9,000 kwa lita kwa mwezi Septemba. Bei ya mafuta ya kupikia haijaonesha mabadiliko ikilinganishwa

na mwezi Agosti. Bei ya chini ya mafuta ya kupikia ipo katika mikoa ya Iringa, Njombe, Manyara, Dodoma, Singida na Songwe na bei ya juu imeripotiwa kwenye mikoa ya Lindi, Pwani na Tabora.

### (h) UNGA WA NGANO

Bei ya unga wa ngano ni kati ya Shilingi 2000 na 2,500 kwa kilo kwa mwezi Septemba. Bei ya chini ya unga wa ngano haijaonesha mabadiliko wakati bei ya juu imeongezeka kwa shilingi 1,500 ikilinganishwa na bei ya mwezi Agosti ambayo ilikuwa kati ya shilingi 2,000 na 4,000. Bei ya chini ya unga wa ngano ya Shilingi 2,000 ipo kwenye mikoa mingi nchini; wakati bei ya juu ipo kwenye mikoa ya Kagera, Arusha, Mbeya na Songwe.

### (i) SUKARI

Bei ya sukari ni kati ya Shilingi 2,500 na 3,000 kwa kilo kwa mwezi Septemba. Bei ya sukari haijaonesha mabadiliko ikilinganishwa na mwezi Agosti. Bei ya chini ya sukari kwa mwezi Septemba ipo katika mikoa ya Kilimanjaro na Tanga; wakati bei ya juu ipo kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Katavi, Kagera, Pwani, Rukwa na Ruvuma. Jitihada za Serikali za kuvutia uwekezaji kwenye uzalishaji wa sukari zimeanza kuzaa matunda kwa kuongezeka kwa kiasi cha sukari kinachozalishwa nchini baada ya upanuzi wa viwanda vilivyopo vya Kilombero na Kagera na ufunguzi wa kiwanda kipya cha sukari cha Bagamoyo. Ongezeko hilo la uzalishaji linatarajiwa kuendelea kupunguza pengo la uzalishaji na kuongeza uhimilivu wa bei ya sukari nchini.

**Nini maana ya takwimu hizi za uzalishaji wa bidhaa za vyakula??** Tafsiri ya takwimu hizi za uzalishaji wa bidhaa za vyakula ni kwamba chakula kipo cha kutosha ndani ya Taifa letu kama takwimu zilivyoonyesha, hivyo hatuna upungufu wa chakula na Serikali inaendelea kufuatilia upatikanaji wa bidhaa za vyakula kwenye masoko yote Nchini. Hata hivyo, kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa hizi ukilinganisha na mwaka jana lazima kutakuwa na mabadiliko kidogo ya bei za bidhaa hizi sokoni ukilinganisha na kipindi kama hiki mwaka jana kwani tupo kwenye biashara ya soko huria. Hii ni kanuni ya kawaida kabisa ya kiuchumi sokoni (The price is determined by market forces DD & SS).

## III. MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA NYINGINE MUHIMU

### a) GESI YA KUPIKIA

Bei ya gesi yenye ujazo wa kilo 15 ni kati ya Shilingi 53,000 na 60,000 kwa mwezi Septemba. Bei ya chini ya gesi ipo katika mikoa ya Kilimanjaro, Tabora na Mbeya; wakati bei ya juu ipo kwenye mikoa ya Kagera, Shinyanga, Simiyu na Ruvuma.

### b) SABUNI ZA MCHE

Bei ya sabuni za mche ni kati ya Shilingi 2,000 na 5,000 kwa mwezi Septemba. Bei ya chini imepungua kwa shilingi 1000 na bei ya juu imepanda kwa shilingi 500 ikilinganishwa na bei ya mwezi Agosti ambayo ilikuwa ni kati ya shilingi 3,000 na 4,500. Bei ya chini ya sabuni za mche kwa mwezi Septemba ipo katika mikoa ya Katavi na Kigoma; wakati bei ya juu ipo kwenye mikoa ya Kagera, Iringa na Mtwara.

## C. HITIMISHO

Ninapenda kuhitimisha taarifa yangu kwa kuuhakikishia umma wa watanzania kuwa, Serikali inaendelea kufuatilia na kufanya tathmini ya bei za bidhaa muhimu ili kuwalinda watumiaji, wazalishaji, na wafanyabiashara wa bidhaa husika. Aidha, Serikali itaendelea kufanya majadiliano na wasambazaji wa bidhaa na wenye viwanda kwa lengo la kuhimiza umuhimu wa kuongeza ufanisi kwenye mifumo ya usambazaji wa bidhaa ili kupunguza gharama za usafirishaji na usambazaji wa bidhaa na hivyo kupunguza tofauti ya bei kati ya mikoa yenye viwanda na mikoa ya pembezoni. Lengo ni kufuata mfumo wa usambazaji unaotumiwa na wazalishaji wa baadhi ya bidhaa unaohakikisha usawa wa bei ya mlaji wa mwisho kwenye mikoa yote.

..................................................

**Dkt. Ashatu K. Kijaji (Mb)**
**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**
**15 SEPTEMBA, 2022**